JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA

SHULE YA SEKONDARI KORONA,
S. L. P. 13402,
ARUSHA.

TAREHE …….

NAMBA YA MKUU WA SHULE: 0754 612090
NAMBA YA MAKAMU WA SHULE: 0768735043

JINA ……..

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2018

1. Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2018, tahasusi ya CBG Shule ya Sekondari Korona ipo umbali wa kilometa 17.5 kutoka Arusha Mjini. Usafiri wa basi kutoka mjini Arusha unapatikana Stendi ya kilombero na nauli ni Tshs. 500/=.kwa daladala na teksi 20,000/=
2. Unatakiwa kufika shuleni tarehe ..... bila kukosa wala kuchelewa tayari kuanza masomo ya kidato cha TANO. Muhula wa masomo unaanza tarehe..... Mwisho wa kuripoti ni tarehe.....
3. Muda wa kuripoti ni kabla ya saa kumi na mbili jioni, baada ya muda huo hautapokelewa.
4. Shule hii ni ya bweni kwa wavulana pekee wa kidato cha tano na sita. Shule ina wanafunzi wa kutwa kwa kidato cha kwanza mpaka cha nne.

MAAGIZO YA KUTIMIZA KABLA YA KUFIKA SHULENI

1. Iwapo unakubali nafasi hii tafadhali jaza fomu zote zilizoambatanishwa na kusaini kila unapopaswa kisha uje nazo shuleni na kuzikabidhi kwa makamu mkuu wa shule.
2. Njoo na ‘pay-in-slip ya’ Benki kwa uthibitisho wa malipo yote uliyoyafanya banki.
3. Njoo na ‘result slip’ ya matokeo yako ya kidato cha nne.
4. Mwanafunzi aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa kwa uthibitisho wa uraia.

VIFAA/MAHITAJI YA LAZIMA UNAYOTAKIWA KULETA

1. Karo (ADA) ni Tsh. 35,000/= kwa muhula na Tsh. 70,000/= kwa mwaka. Ada hii ni muhimu ilipwe kwenye akaunti ya shule iliyopo **NMB Clock Tower 4081200307**
N.B: Pesa hazitapokelewa shuleni.
2. Godoro linapatikana shuleni utaliazima na kulipia TZS 40,000/- kwa miaka miwili, fedha hizo ziwekwe kwenye akaunti ya michango mingine **NMB (4081200306)**
3. Mwanafunzi ambaye hatakuja na pay-in-slip zinazoonyesha malipo aliyofanya banki hatapokelewa shuleni.

MICHANGO MINGINE ILIPWE BANK YA NMB AKAUNTI NA. 4081200306

1. Tahadhari Tsh. 5,000/= (hairudishwi)
2. Kitambulisho Tsh. 6,000/=
3. Mchango wa wahudumu (walinzi, karani, mkutubi, wapishi) Tsh. 60,000/= kwa mwaka
4. Taaluma Tsh. 20,000/= kwa mwaka
5. Nembo ya shule Tsh. 2,000/=
6. Matibabu Tsh. 15,000/= (Huduma ya kwanza na Bima ya Afya) kwa mwaka
7. Ukarabati wa samani Tshs. 30,000/= kwa mwaka
8. Mitihani ya kujipima Tshs. 20,000/= kwa mwaka

SARE YA SHULE

1. Mashati meupe mawili (2) ya mikono mirefu na isiyo na urembo wowote.
2. Suruali mbili za rangi ya ugoro iliyokolea (dark brown) mbili, pia zinapatikana shuleni kwa Tsh. 15,000/= kila moja.
3. Sweta rangi kama ya suruali dark brown (Kenya) pia zinapatikana shuleni kwa Tsh. 17,000/=.
4. Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba visivyo na visigino virefu.
5. Tai rangi ya ugoro (rangi ya suruali) yenye mistari meupe, pia zinapatikana shuleni kwa Tsh. 3,000/=
6. Soksi nyeusi njozi mbili.
7. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia unifomu.

MAHITAJI MENGINE YA SHULE

1. Rim mbili (2) za karatasi za photocopy.
2. Nguo za michezo, raba nyeusi, bukta ya dark green, T-shirt dack green
3. Track suit ya maroon jozi mbili(2) zisizo na maandishi wala picha yoyote waweza zinunua shuleni kwa TZS 30,000/-kwa jozi moja .
4. Shuka mbili rangi ya blue .
5. Blanketi moja (1) zito.
6. Mto na foronya (rangi ya blue).
7. Nguo za kulalia.
8. Sanduku Ia chuma lenye kufuli imara kwa ajili ya kuhifadhia vifaa vyako.
9. Bakuli, sahani, kikombe na kijiko (visiwe vya plastiki).
10. Ndoo lita 20, 1 na lita 10, 1(zenye mifuniko); Hard broom 1; rubber squeezer 1; jembe kubwa 1; Reki 1; Toilet brush1na soft broom 1 kwa ajili ya usafi.
11. Madaftari ya kutosha (counter books) 4 quires.
12. Scientific calculator na mathematical set.
13. Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia.

VITABU:
Ifuatayo ni orodha ya vitabu vinavyotumika darasani. Mwanafunzi ajitahidi kuwa navyo angalau baadhi.

I. **MATHEMATICS**

- Pure Mathematics - K. J Backhouse
- Advanced level mathematics - L.K. Shayo.

II. **GEOGRAPHY**

- Landforms in Africa: By Colin Buckle
- Principles of Physical Geography: By Monkhouse
- Geography Integrated Approach: By Waugh
- Practical Geography for Africa: By J. M Pritchard
- Africa: By J. M. Pritchard
- Tropical lands: By Michael Seniar.
- Human and Economic Geography: By Morgan.
- Geography dictionary by …..

III. **BIOLOGY**

- Biological science: By Taylor
- New understanding biology: By Glenn & Suzan Toole
- Biology: by Chand

IV. **CHEMISTRY**

- Conceptual chemistry xi & xii: By Chand
- Chemistry books for advanced: Mzumbe book project

……..…

NNYARI L. M

MKUU WA SHULE

MASHARTI YA KUZINGATIA WANAFUNZI WOTE WA BWENI

1. Wanafunzi wale waingiao bweni wanapaswa kufuata masharti yote ya shule.
2. Usafi wa bweni ni wajibu wa kila mwanafunzi anayeishi kwenye bweni.
3. Kila mwanafunzi aheshimu kazi za mikono zote mbili ikiwa ni pamoja na bustani za maua, usafi wa mazingira na anapaswa kuheshimu masorno ya darasani.
4. Kila mwanafunzi aheshimu na kutunza mali za shule, uharibifu wowote utakaotokea ndani ya bweni itabidi ugharamiwe na mwanafunzi mwenyewe.
5. Ugomvi wa maneno, matusi, kupigana ni mwiko.
6. Ruhusa zote za kulala nje ya shule zitatolewa na Mkuu wa shule au Makarnu wake tu.
7. Ni lazima kuzima taa saa 4:00 usiku na kulala,
8. Mwanafunzi hatakiwi kubaki bweni wakati wa masomo bila taarifa au ruhusa ya mwalimu wa zamu au patron.
9. Kelele zisizo na maana ni mwiko ndani ya bweni.
10. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kutumia vyombo vya umeme kama vile heater, radio, pasi ya umeme, jiko ndani ya bweni au kufanya ufundi wa aina yoyote kwenye umeme ndani ya bweni na darasani.
11. Mwanafunzi yeyote haruhusiwi kwenda nyumbani kwa mwalirnu au mfanyakazi asiye mwalimu bila ruhusa.
12. Ni marufuku mwanafunzi kuwa na vifaa vyenye ncha kali au vitu vinavyolipuka na dawa za aina zozote ndani ya bweni.
13. Ni marufuku kwa mwanafunzi wa bweni kubaki ndani ya bweni au kuzurura nje wakati wa preparation (saa 2:00 usiku — 4:00 usiku).
14. Siku ya kutembelea wanafunzi wa bweni ni jumamosi ya kwanza ya mwezi kuanzia saa 7 mchana mpaka 10:00 jioni na wageni wote wataingia ofisi ya mwalimu wa zamu.

(A) MAVAZI

I. Nguo za binafsi haziruhusiwi shuleni kabisa.
II. Wanafunzi wote wa bweni wanatakiwa muda wote wavae sare za shule (shamba dress) baada ya masomo hawaruhusiwi kuvaa nguo nyingine tofauti na sare zinazotakiwa.
III. Wanafunzi wa bweni wanatakiwa wawe na mashuka mawili ya blue yasio na maua (plain) blanketi 1), mto 1 na sanduku 1 la bati.

(B) CHAKULA

I. Wanafunzi wa bweni watapata chakula cha kawaida kufuatana na kiwango cha fedha kinacholipiwa.
II. Wanafunzi wote wanatakiwa wawe na sahani 1, bakuli 1, kikornbe, kijiko 1 (visiwe vya plastiki)

(C) MATIBABU

Taratibu za huduma ya kwanza zitapangwa na Mkuu wa shule pindi mwanao atakapojiunga na bweni aidha endapo mwanafunzi ataugua mzazi atagharamia matibabu.

SAINI YA MWANAFUNZI…….. **TAREHE……..**

SAINI YA MZAZI / MLEZI …… **TAREHE ……..**

SHERIA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazirna.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule.
3. Ni muhimu kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (preparation)
4. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
5. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
6. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Kutokuhudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
3. Kugoma na kuhamasisha mgomo
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga/kutishia kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
6. Ulevi au unywaji wa pombe.
7. Uvutaji wa sigara, bangi na matumizi ya madawa ya kulevya.
8. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja.
9. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
10. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
11. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi, charger au laini ya simu katika mazingira ya shule.
12. Kudharau bendera ya Taifa.
13. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
14. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.
15. Kutoroka shule.

16.Kutokuvaa sare ya shule

SHULE YA SEKONDARI KORONA

FOMU YA KUKUBALI NAFASI NA UTII

1. Mimi……. (Jina kamili) Kidato cha……..... mwaka ……. natambua wajibu wangu kama mwanafunzi kwa Taifa na jamii kwa ujumla na ninaahidi kwamba:
   A. Nitafuata sheria na kanuni zote za shule pamoja na maelekezo yote yanayotolewa mara kwa mara na uongozi wa shule.
   B. Nitatii na kuheshimu viongozi wangu wote kuanzia viongozi wa darasa, viranja, watumishi wote wasio walimu na walimu hadi mkuu wa shule.
   C. Sitatoka nje ya mipaka ya shule wakati wote nitakapokuwa shuleni labda tu kwa shughuli maalumu na baada ya kupata kibali kwa maandishi kutoka kwa Mwalimu au Mkuu wa Shule mwenyewe.
   D. **Sitagoma wala kusababisha mgomo wowote** kwa kipindi chote nitakapokuwa nikisoma katika shule hii.
   E. Kama nitashindwa kufuata hayo yote hapo juu, hatua kali za nidhamu zichukuliwe dhidi yangu ambayo ni pamoja na kusimamishwa masomo au kufukuzwa shule.

TAREHE…… **……**

JINA NA SAINI YA MWANAFUNZI

2. Mimi …….. Mzazi /Mlezi wa……...
   Nimesoma na kuelewa /kukubaliana na sheria na kanuni za shule. Endapo mtoto wangu atashindwa kufuata hayo yote hatua kali dhidi yake zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kusimamishwa masorno au kufukuzwa shule.
   Pia nitakuwa mwaminifu kutoa ada na michango yote iliyokubaliwa kisheria bila usumbufu na kuhakikisha mtoto wangu anapata mahitaji yote ya muhimu.

TAREHE …….. **…….**

JINA NA SAINI YA MZAZI / MLEZI

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI ……...

3. **Mimi …… (jina la mwenyekiti wa mtaa/kijiji) mwenyekiti wa mtaa/kijiji …… (taja jina la mtaa/kijiji), nathibitisha kuwa Ndugu …… ni Mzazi/mlezi wa mtoto huyu aliyechaguliwa kujiunga kidato cha tano.**

   Maoni/mapendekezo kuhusiana na unavyomfahamu mwanafunzi huyu: ……

   ……

   Sahihi ya mwenyekiti wa mtaa/kijiji …… Tarehe ……...

   Namba ya simu …… Mhuri ……..

4. **Jina la Mtendaji Kata …….**

   Kata ya …… Sahihi ya Mtendaji Kata .....

   Namba ya simu ya Mtendaji Kata .....

   Tarehe ..... Mhuri .....

SHULE *YA* SEKONDARI MRINGA

FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI

HABARI ZA MZAZI / MLEZI

1. Jina kamili Ia Baba ……..
2. Kazi yake……..
3. Jina kamili la Mama…….……
4. Kazi yake…….…….
5. Jina kamili Ia Mlezi (iwapo mtoto haishi na wazazi wake) ……..
6. Kazi na anwani ya mIezi …….....
7. Nyumbani kwa Baba (alipozaliwa mtoto) Kijiji /Mtaa.....

   Wilaya……..……..... Tarafa ……....

   Kata..... Mkoa .....
8. Anwani ya mahali pa kazi ya baba……..
   Namba ya simu……
9. Anwani ya mahali pa kazi ya mama……...
   Namba ya simu…….
10. Mtoto anaishi na (I) Baba tu (ii) Mama tu (iii) Wazazi wote (iv) Walezi **(Kata isiyohusika)**
11. Dini ya baba …… Dhehebu ……
    Dini ya mama …….. Dhehebu …….
    Dhehebu unalotaka mwanao alelewe ……
12. Anwani kamili ya nyumba ambapo mtoto atakuwa anakwenda siku za likizo ……
13. Mimi ……. (Jina la Baba/Mama/Mlezi) wa ……. nathibitisha kuwa taarifa hii hapa juu ni sahihi na naahidi kushirikiana na walimu na uongozi wa shule ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakuwa na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masomo.

TAREHE…….. ……

JINA NA SAINI YA MZAZI/MLEZI

PRESIDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a medical Officer in Government Hospital in respect of all entrants to Korona Secondary School)

Pupil's full name ……

Age ……..

1. Blood count (red and white) ……
2. Stool examinations ……
3. Urinalysis ……
4. Syphilis test ……
5. T.B. test ……..
6. Eye test ……
7. Ears test ……..
8. Chest ……
9. Abdomen ……
10. Spleen ……...

11. Additional information: e.g. physical defect, infection, chronic or family diseases etc
    ……
    ……
    ……

    Treatment after examination…….
    …….
    ……..

(Please state nature of treatment)

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue further studies

Signature ……

Designation ……

Station ……..

Date: …… Official stamp …….